



**OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**



SHULE YA MSINGI ILEMBULA

TANGAZO LA KUMPATA MSIMAMIZI WA MRADI MWENYE FANI YA UJENZI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA PROGRAMU YA BOOST

TAREHE 12/5/2023

Shule ya Msingi **ILEMBULA** imepokea fedha kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule kwa programu ya BOOST ambayo ni ujenzi wa matundu matatu (3) ya vyoo. Aidha kwa mujibu wa muongozo kazi hizi zitasimamiwa na mtaalamu/wataalamu wenye ujuzi,uzoefu na wenye taaluma ya ufundi kwa kazi za ujenzi.

1. Hivyo, wataalamu wote wenye ujuzi,uzoefu na wenye taaluma ya ufundi kwa kazi za ujenzi ndani ya mradi au nje ya mradi wanaalikwa kutuma maombi yao kupitia kwa wasimamizi waliokasimishwa madaraka ya afisa masuhuli katika ngazi ya vituo ambapo katika shule ni mwalimu Mkuu kuanzia tarehe **12/5/2023**
2. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni tarehe 17/5/2023 **saa 7:30** **mchana**.Kotesheni zote zitafunguliwa kwa uwazi mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.

Kotesheni zote lazima zijazwe kikamilifu na kufungwa kwenye bahasha na kuwasilishwa,kupitia..anwani **ifuatayo Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Ilembula**

S.L.P 20 Ilembula.

3. Kotesheni zitakazochelewa na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa.

4.

Jedwali la miundombinu itakayojengwa

Na	AINA YA KAZI	NAMBA YA ZABUNI
1	Ujenzi Wa Matundu Matatu (3) Ya Vyoo	LGA/153/2022/2023/W/8

KAZI ANAZOTAKIWA KUFANYA FUNDI

1.Ujenzi wa mashimo mawili ,shimo la duara na shimo lenye pembe nne lenye vipimo vifuatavyo

(a)Shimo la pembe nne 4.5m x 3.3 m x4 m

(b)Shimo la Duara lenye kipenyo cha 4m x 4,5m

A.Msingi wa jengo (substructure)

B.Kunyanyua Jengo (Super structure)

C.Kuezeka (Roof structure and covering)

D.Milango

E.Umaliziaji (Finishing)

F.Rangi na Mapambo (Painting and Decoration)

G.Umeme (Electrical installation)

H.Mifumo ya maji safi na maji taka.

SIFA ZA WAOMBAJI

- Waombaji wote lazima wawe na taaluma ya ujenzi kutoka vyuo vinavyotambuliwa na seriali katika ngazi ya fundi stadi(VETA daraja la I),Fundi sanifu ngazi ya FTC/Diploma au Shahada
- Uzoefu wa kujenga/kusimamia majengo ya serikali au taasisi kwa muda usiopungua miaka 3
- Ujuzi wa kutafsiri michoro na mchanganuo wa vifaa(schedule of materials)
- Uwezo wa kujisimamia,kusimamia kundi kubwa mafundi na vibarua kwa kuwapangia kazi kwa ukubwa unaostahili(piece work)
- Uwezo wa kuandaa mpango kazi(Working programme)

MAJUKUMU

- Kusimamia kundi kubwa mafundi na vibarua kwa kuwapangia kazi kwa ukubwa unaostahili(piece work)
- Kupima kazi iliyofanywa na mafundi waliopo chini yake kwaajili ya kuombewa malipo
- Kusimamia ubora wa kazi kwaniaba ya mwajiri chini ya Mhandisi wa Ujenzi/Miundombinu(W)

- Kuandaa mpango kazi(Working programme)
- Kuandaa taarifa ya mradi hatua kwa hatua
- Kuandaa malipo kwaajili ya mafundi wa fani tofaauti na vibarua waliopo chini yako
- Kusimamia matumizi ya vifaa vifaa vya mwajiri
- Kutoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa kamati za usimamizi wa mradi
- Kutoa ushauri kwa mwajiri kabla ya kutekelezaji ili ushauri huo ujadiliwe
- Kutunza daftari la kutunza vifaa(site ledger)
- Kutunza daftari la mahudhurio kwa mafundi na vibarua
- Kukaa kwenye eneo la mradi muda wote wa utekelezaji
- Kushirikiana na kamati za mradi kusimamia utendaji

MASHARTI YA UJUMLA

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea
- Asiwe mwajiriwa wa serikali
- Awe hajawahi kushtakiwa
- Aambatishe cheti cha NIDA
- Awe na barua ya utambulisho toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kata

Tanbihi:Mafundi wengine wa fani mbalimbali(uashi,useremala,uchomeleaji,rangi,umeme n.k) watakaosimamiwa na msimamizi mkuu watatuma maombi yao moja kwa moja wakati wa utekelezaji wa mradi eneo la mradi

Fomu ya kujaza gharama za usimamizi(supervision), mafundi na vibarua (schedule of labour)inapatikana kwa **Mwalimu mkuu shule ya msingi Ilembula** kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa

Limetolewa na: Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Ilembula

S.L.P 20 Ilembula.

.....
DORAH YOHANA MWENGA
MWALIMU MKUU

